



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Barua pepe: rbctabora@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 11

TAKUKURU Mkoa,
S. L. P 1020
Tabora

TAARIFA KWA UMMA

TABORA

Agosti, 2024

TAKUKURU YADHIBITI NA KUZUIA UBADHIRIFU WA SHS. 3,053,372,698.31 KWENYE ZABUNI YA UJENZI MKOANI TABORA.

TAKUKURU Mkoa wa Tabora imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2022. Moja ya majukumu hayo ni kuzuia vitendo vya rushwa visitokee na kusababisha madhara ndani ya jamii.

Katika kipindi cha Aprili - Juni 2024 TAKUKURU Tabora imefanikiwa kuzuia vitendo vya rushwa kwa kuokoa jumla ya Shs 3,053,372,698.31 kwenye zabuni ya mradi wa ujenzi wa stendi na soko kuu la Manispaa ya Tabora. Pamoja na udhibiti huo, TAKUKURU inaendelea na uchunguzi ili kuweza kuchukua hatua za kisheria kwa wote watakaobainika kuhusika na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Manunuzi kwenye zabuni hiyo.

UZUIAJI RUSHWA

Wakati huo huo tumefanya ukaguzi wa miradi 23 ya maendeleo yenye thamani ya shilingi 9,114,830,038/-. Kati ya miradi iliyokaguliwa miradi 4 yenye thamani ya shilingi 1,668,206,695 ilikutwa ina mapungufu mbalimbali ambayo yalifanyiwa marekebisho ili miradi hiyo iakisi uhalisia wa thamani na mahitaji yaliyokusudiwa. Pia tumefanya chambuzi za mifumo 8, warsha 8, na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati iliyowekwa kutokana mapendekezo yaliyotolewa na TAKUKURU

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU.TZ



TAKUKURU APP

113

(Compliance check) 12 ambapo katika ufuatiliaji huu kulikuwa na mapendekezo **107** yaliyotolewa kwa kipindi tajwa na mapendekezo **99** (92.5%) yametokelezwa katika taasisi husika ili kuziba mianya ya rushwa. Aidha, Chambuzi zilizofanyika ni katika sekta za Afya, Elimu, Uhifadhi wanyama pori, na Biashara kama inavyoonekana kwenye majedwali ya ufafanuzi kwenye viambatisho.

ELIMU KWA UMMA

Kwa kipindi cha Aprili - Juni 2024 tumetoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa na dawa za kulevya kupitia uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa, mikutano ya hadhara na vipindi vya redio. Kumekua na mashirikiano kati ya ya TAKUKURU na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule za Msingi kwenye michezo ya UMISETA iliyofanyika katika Mkoa wa Tabora. Kazi zilizofanyika ni pamoja na semina 35, mikutano ya hadhara 90, kufungua na kuimarisha klabu 82, vipindi vya redio 06 na onesho 1.

UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Malalamiko 114 yalipokelewa kwenye ofisi zetu, ambapo malalamiko 95 yalihusu rushwa ambayo uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali, taarifa 3 zilihamishwa kwenda kwenye mamlaka nyingine ili zifanyiwe kazi, na watoa taarifa 4 walipewa ushauri wa kutatua malalamiko yao. Jumla ya taarifa 12 uchunguzi wake ulifungwa baada ya kukosa ushahidi.

Kwa upande wa mashtaka jumla ya kesi mpya 7 zilifunguliwa na jumla 4 Jamhuri ilishinda.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI

Kwa kipindi cha Aprili -Juni 2024 TAKUKURU Tabora imefanikiwa kufanya Programu ya TAKUKURU Rafiki kwa kufanya vikao katika Kata 26. Katika vikao hivyo jumla ya Kero 306 zilibuliwa na kero 261 (85.2%) zimetatuliwa katika kipindi tajwa. Aidha, Vikao 51 vilifanyika katika Kata mbalimbali ili kupeleka mrejesho wa utatuzi wa kero zilizoibuliwa katika vikao hivyo. Baadhi ya kero zilizoibuliwa zilitoka katika sekta mbalimbali kama Miundombinu (Barabara), Nishati, Elimu na Afya.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU;TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU.TZ



TAKUKURU APP

113

MIKAKATI YA JULAI – SEPTEMBER 2024

Kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2024 tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa mujibu wa Sheria. Mkazo mkubwa utakua Kuzuia vitendo vya rushwa kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Tutashirikiana na wadau mbalimbali wa uchaguzi katika kuzuia vitendo vya rushwa visitokee kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi.

WITO KWA WAKAZI WA MKOA WA TABORA

Ninawakumbusha wakazi wa Mkoa wa Tabora kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa. Endeeleni kuleta taarifa za vitendo vya rushwa ili tuweze kuzuia madhara yanayoweza kuletwa na uwepo wa vitendo hivyo.

"KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU"

Imetolewa Na:



ABNERY MGANGA
MKUU WA TAKUKURU Mkoa wa TABORA
0738 - 150218

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU
TV



TAKUKURU.TZ

Download on the
App Store

GET IT ON
Google Play

TAKUKURU APP

113

KAZI ZA UZUIAJI RUSHWA

Jedwali Na. 1: UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Na.	UFUATILIAJI WA YA MAENDELEO	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1	Ufuatiliaji Wa Mradi Wa Ujenzi Mfumo Wa Maji Taka Unaotekelezwa Na IGUWASA katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga	Uchelewashaji wa malipo ya Mkandarasi uliosababisha Uchelewashaji wa mradi.	Mkandarasi alilipwa malipo yote aliyokuwa anadai.
2	Ujenzi wa Madarasa Matano na matundu 8 ya vyoo katika Shule ya Sekondari Itonjanda Katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora	Mzabuni aliandika bei iliyohusisha VAT kwenye mfumo wa NEST Kulikua na ukadriaji mara mbili ya kodi ya VAT (Double VAT) kwenye Mkataba mmoja.	Mzabuni alishauriwa kuondoa double quoting ya VAT kwenye mkataba na mzabuni alifanya hivyo.
3	Ufuatiliaji wa mradi wa Boost, ujenzi wa shule mpya ya msingi Kipugila wenye thamani ya shilingi 361,500,000.00 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega	Kuongeza tofali nje ya makisio ya BOQ tofali 7241 zenye thamani ya shilingi 11,585,600.00	Uchunguzi umeanzishwa
4	Ujenzi Wa Shule Mpya Ikonongo Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua	Ufitishaji mbovu wa dirisha za Aluminium (Madirisha yaliyotengezwa	Mhandisi msimamizi wa mradi ameshauriwa apitishie malipo baada ya marekebisho kufanyika.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/**113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU.TZ



TAKUKURU APP SMS 113

		yalikuwa hayalingani)	Marekebishi ya madirisha yalifanyika na kufitishwa inavyopaswa.
--	--	-----------------------	---

Jedwali Na. 2: UCHAMBUZI WA MIFUMO

S/N	UCHAMBUZI WA MFUMO	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1	Uchambuzi Wa Mfumo Wa Matumizi Ya Mfumo Wa TEHAMA (GoTHOMIS) Katika Kituo Cha Afya Mailitano Manispaa ya Tabora	<p>Utunzaji hafifu wa kumbukumbu za makusanyo ya mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa katika kituo hicho</p> <p>Utaratibu mbaya wa ukusanyaji mapato katika kituo uliopelekea fedha kukusanywa bila kuwasilishwa Benki katika akaunti ya Kituo.</p> <p>Matumizi ya nywila kwa Zaidi ya mtu mmoja</p>	<p>Kikao kazi kiliazimia kuwasimamia na kuwahimiza watumishi wa Kituo hicho kutumia mfumo wa GoTHOMIS kwa uaminifu na kuwasilisha fedha zote benki kwa wakati.</p> <p>Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati uliowekwa ulibaini ukusanyaji wa mapato umeimarika na kuongezeka hadi kufikia kiasi cha Shs.8,563,800/= kwa kipindi cha miezi minne ongezeko la kiasi cha Shs.7,109,800/= ukilinganisha na kipindi cha nyuma kabla ya uchambuzi huu ambapo makusanyo yalikuwa wastani wa 1,454,000 kwa mwezi.</p> <p>TAKUKURU (M) wa Tabora imechangia kwa kiasi kikubwa</p>

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU.TZ



App Store



Google Play

TAKUKURU APP

113

			kuimarisha matumizi ya mfumo katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na utoaji wa huduma za afya kituoni hapo.
2	Mfumo wa mapato yatokanayo na uhifadhi katika jumuiya ya hifadhi wanyamapori Ipole	<p>Kushindwa kufuata taratibu za fedha kwa Kukosekana kwa utunzaji mzuri wa kumbukumbu hasa mihutasari ya kutoa fedha benki.</p> <p>Kukusanya mapato kutumia bila kutumia POS Machine.</p> <p>Wafugaji kuingiza mifugo hifadhini.</p> <p>Sheria ndogo za Halmashauri za kuhifadhi wanyapori 2008 na Katiba ya mwaka 2006 ilionekana kupitwa na wakati.</p>	<p>Kilifanyika Kikao kazi kilifanyika kujadili na kuweka mikakati kutataua yaliyobainika.</p> <p>Jumuiya ziliomba POS kupitia halmashauri ili iweze kutumika Kuanzia mwaka wa fedha unaoanzia Julai 2024 kutumia Machine katika ukusanyaji wa mapato.</p> <p>Wafugaji walipewa elimu na wameacha kuingiza mifugo hifadhini.</p> <p>Mchakato wa kurekebisha sheria ndogo kupitia mwanasheria wa Halmashauri uliashanza.</p>
3	Uchambuzi wa Mfumo ukusanyaji mapato katika Vizuizi	<p>- Vizuizi vyote havina nakala za sheria za ada na ukusanyaji wa ushuru</p> <p>-Kukosekana miongozo inayoonesha adhabu</p>	Kikao kilifanyika na watu wa Halmashauri na kupewa maelekezo ya Kuwekwa sheria za ada na ushuru pamoja na mabango yanayoonesha adhabu kwa watu wanaokiuka taratibu za vizuizi hivyo.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU.TZ



TAKUKURU APP 113

		kwa wanaokiuka taratibu za vizuizi hivyo.	Mapendekezo hayo yameanza kufanya kazi.
--	--	---	---

UJELIMISHAJI UMMA

Jedwali Na. 3: KAZI ZA ELIMU KWA UMMA

Kazi	Semina	Utoaji wa Habari na Makala	Mikutano Ya Hadhara	Vipindi Vya Redio Na Tv	Kufungua Kuimarisha Za Rushwa	Na Kluba wapinga	Maonesho
Idadi	35	16	90	6	82		1

Jedwali Na. 4: UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU Rafiki: Katika

Utambuzi na utatuzi wa kero

Mkoa	Wilaya	Idadi ya kata zilizofikiwa	Idadi ya kero zilizoibuliwa	Idadi ya kero zilizotatuliwa	Idadi ya kero ambazo hazijatatuliwa	Idadi ya vikao vya mrejesho
Tabora	Mkoani	4	86	74	12	10
	Igunga	4	17	13	4	12
	Uyui	6	98	94	4	6
	Sikonge	3	35	30	5	6
	Urambo	2	17	8	9	5
	Kaliua	7	53	42	11	0
	Nzega					12
Jumla		26	306	261 (85.2%)	45 (14.8%)	51

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU APP

App Store Google Play

TAKUKURU APP 113

MIFANO YA KERO ZILIZOTATULIWA NA SEKTA YAKE KTK MABANO	MAFANIKIO YA TAKUKURU RAFIKI KATIKA MKOA WAKO KWA KIFUPI
Ujenzi wa Barabara ya Itetemia - Kwihara umechukua muda mrefu na mkanadarsi ameitelekeza site na mpaka sasa barabara hiyo haijakamilika.	- Kero hiyo iliwasilishwa TARURA ambao walimwandikia barua mkandarasi huyo na kumchaji gharama za ucheleweshaji wa ujenzi wa barabara hio. Kwa sasa mkandarasi huyo amerudi site na anaendelea na kazi.
Vitongozi vya Kata ya Ndevelwa vingi havijaunganishiwa Umeme kwa muda mrefu.	- TANESCO wameeleza kuwa vitongozi hivyo vitaunganishiwa umeme wa REA katika mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024-2025
Ubovu wa barabara ya Ndevelwa - Tabora Mjini kwa muda mrefu	- Mkandarasi alisimama ujenzi wa barabara kutokana na mvua na ilielezwa amerudi site mwezi wa sita mwishoni na bajeti ya upanuzi wa kipande cha barabara hiyo itatolewa kwa mwaka 2024-2025.

Jedwali Na 5: UCHUNGUZI NA MASHITAKA

NA.	YANAYOHUSI RUSHWA	YASIYOHUSU RUSHWA
1	MALALAMIKO YALIYOPOKELEWA	95
2	HATUA ZILIZOCHUKULIWA	Uchunguzi unaendelea 04 - Watoa taarifa wamishauriwa 03- Yamehamishiwa Ishara zingine

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMKOE WAJIBU WETU



113/4113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU
TV



TAKUKURU
APP



TAKUKURU
APP



TAKUKURU APP SMS 113

		12 - Majalada yamefungwa
	SEKTA ZILIZOLALAMIKIWA	Halmashauri/Serikali za Mkoa 83, Polisi 5, Afya 8, Ardhi 3, Ujenzi 11, Ushirika 4
4	MAJALADA YALIYOKAMILIKA	15
5	MAJALADA YALIYOPATA KIBALI CHA DPP	5
6	KESI MPYA ZILIZOFUNGULIWA MAHAKAMANI	7
7	KESI ZILIZOTOLEWA MAAMUZI NA JAMHURI KUSHINDA	4
8	KESI ZINAZOENDELEA MAHAKAMANI	16

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU



113/*113#



Takukuru Tz



takukuru.tz



TAKUKURU TV



TAKUKURU



TAKUKURU APP

113